

# TAARIFA YA MKUTANO WA PILI WA WADAU WA ZAO LA PARACHICHI

TAREHE: 25 SEPTEMBA, 2025

# Yaliyomo


1. UTANGULIZI
2. HOTUBA YA MGENI MGENI RASMI
3. UJUMBE WA VIONGOZI
4. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO WA KWANZA WA KITAIFA WA ZAO LA PARACHICHI APRILI, 2025.
5. MAWASILISHO
6. MAJADILIANO.
7. MAAZIMIO
8. HITIMISHO




# 1. UTANGULIZI


Parachichi ni miongoni mwa mazao ya kimkakati nchini Tanzania yenye mchango mkubwa katika kuliingizia taifa fedha za kigeni, kuimarisha mapato ya wadau katika mnyororo wa thamani na kuongeza pato la taifa. Uzalishaji wa zao hili umeendelea kuimarika ambapo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 na 2023/202 uzalishaji umeongezeka kutoka tani 188,712hadi tani 198,162. Aidha, katika kipindi hicho, mauzo ya nje yameongezeka kutoka tani 17,711 hadi tani 35,627.02 yenye thamani ya Shilingi bilioni 117.53 na Shilingi bilioni 252.27 mtawalia.



*Bi. Irene M. Mlola, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Nafaka na Mazao Mchanganyiko.*

Pamoja na mafanikio hayo, tasnia ya parachichi bado inakabaliwa na changamoto zikiwemo kutokuwepo kwa uwazi na usawa katika soko la ndani, hali inayomsababishia mkulima kupata bei ndogo na kutokunufaika na uzalishaji wa zao hilo. Aidha, changamoto nyingine ni pamoja na uhaba wa miundombinu ya umwagiliaji, ubovu wa barabara za mashambani, ukosefu wa miundombinu ya kukusanya na kuhifadhi parachichi, matumizi duni ya pembejeo na kanuni za kilimo bora cha parachichi. Changamoto hizo zimekuwa zikiathiri ubora wa parachichi, ukosefu wa masoko na kuchangia upotevu.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kwa kushirikiana na TAHA, na Wadau wa zao hilo, iliandaa Mkutano wa Pili wa Wadau wa Zao la Parachichi uliofanyika tarehe 25 Septemba, 2025 katika ukumbi wa Hoteli ya Agreement mkoani Njombe. Mkutano huo uliongozwa na kauli ya "Msimu Mpya, Fursa Mpya, Parachichi kwa Maendeleo ya Tanzania". Mgeni Rasmi wa mkutano huo alikuwa Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa mkutano huo.





## 1.1 Malengo ya Mkutano

Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kufungua rasmi msimu wa ununuzi wa parachichi kwa mwaka 2025/2026. Aidha, malengo mahsusi yalikuwa ni pamoja na;

- Kuwasilisha urasimishaji wa usimamizi wa biashara ya zao la parachichi ikijumuisha; wasilisho la kalenda ya msimu (msimu mdogo na mkubwa), rasimu ya Kanuni za Usimamizi ya zap la Parachichi; usajili wa wanunuzi na wakala wa ununuzi, utambuzi wa wavunaji, utaratibu wa kupata kibali cha uvunaji, utambuzi wa madaraja (Daraja la kwanza, Daraja la pili na Daraja la viwandani, Kiambatisho Na. 1), uanzishwaji wa vituo vya kukusanyia na kununua parachichi (collection and buying centers) na usimamizi wa bei ya parachichi,
- Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Wadau wa zao la Parachichi uliofanyika tarehe 4 Aprili, 2025 Jijini Dodoma, na
- Kuibua na kupokea mapendekezo ya kisera yatakayowezesha kutatua changamoto na kusaidia ukuaji endelevu wa tasnia ya parachichi nchini.

## *1.2 Ajenda za Mkutano*

a) Kufungua rasmi msimu wa ununuzi wa parachichi kwa mwaka 2025/2026.
b) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Wadau wa zao la Parachichi wa Aprili 2025.
c) Kupokea mawasilisho kuhusu maendeleo na usimamizi wa tasnia ya parachichi nchini.
d) Majadiliano.
e) Kufunga mkutano.

## *1.3 Washiriki wa Mkutano*

Jumla ya wadau 425 walishiriki mkutano huo kutoka makundi mbalimbali ya kiwemo:
i.Viongozi na Maafisa kutoka taasisi za Serikali na Binafsi,
ii.Wakuu wa Wilaya kutoka mikoa ya uzalishaji wa parachichi,
iii.Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala Wasaidizi Uchumi na Uzalishaji, Maafisa Kilimo ngazi ya Mkoa na Wilaya kutoka mikoa ya uzalishaji wa parachichi,
iv.Vyama vya wakulima (AMCOS na Vikundi) kutoka mikoa ya uzalishaji wa parachchi,
v.Wanunuzi na wachakakaji,
vi.Wabia wa maendeleo,
vii.Taasisi za kifedha,
viii.Taasisi za mawasiliano, na
ix.Waandishi wa vyombo vya habari.

## *Kufungua Mkutano na Salamu za Viongozi*

Mkutano wa Pili wa Kitaifa wa wadau wa zo la parachichi ulifunguliwa na Mhe.Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa Njombe, ambapo kabla ya ufunguzi rasmi Bi. Irene M. Mlola, Mkurugenzi Mkuu wa COPRA aliwatambulisha washiriki na kuelezea muundo wa mkutano.
1.4 Salamu za Viongozi
Viongozi mbalimbali walipata nafasi ya kutoa salamu kama ifuatavyo;
1.4.1 Salamu kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa wa Njombe
Bi.Judica H. Omari, Katibu tawala Mkoa wa Njombealitoa salamu kwa niaba ya Makatibu Tawala kutoka mikoa yote inayozalisha parachichi nchini. Bi.Judicaalipongeza Wizara ya Kilimo na COPRA kwa kuchagua Njombe kuwa mwenyeji wa mkutano wa pili wa wadau wa zao la parachichi.

## 2. HOTUBA YA MGENI MGENI RASMI

Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe na Mgeni Rasmi katika hotuba yake alisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirikiano na kutumia kikamilifu fursa zilizopo katika soko la kimataifa la parachichi. Miongoni mwa masuala muhimu aliyozungumzia ni changamoto ya uwepo wa mageti mengi ya kutoza ushuru wakati wa usafirishaji wa parachichi.

Mgeni rasmi alitoa wito kwa Wakurugenzi Watendaji katika maeneo ya uzalishaji kuhakikisha wanaweka mazingira wezeshi kwa wakulima, ikiwemo kuboresha miundombinu, ili ukusanyaji wa mapato uendane na kiwango cha uwekezaji na usiwe mzigo kwa wadau. Vilevile, aliahidi kuwa suala hilo litashughulikiwa kwa ukamilifu.

Akiendelea na hotuba yake, Mheshimiwa Mtaka aliwataka Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kuwa tasnia ya parachichi inaendeshwa kwa utaratibu unaolinda maslahi ya wakulima na wafanyabiashara. Akitaja zao la parachichi kama "*lulu ya Njombe*", alihimiza wakulima kuuza mazao yao kwa wakati ili kuepuka kuharibika na kupoteza ubora jambo ambalo linaweza kuathiri ushindani wa parachichi ya Tanzania katika soko la kimataifa.

Aidha, alitoa wito maalumu kuhusu ukusanyaji wa ushuru, akisema: "Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi, tengenezeni utaratibu mzuri wa kushughulikia zao la parachichi hasa linapofika getini. Muwe na mfumo wa ukusanyaji ushuru usiowakandamiza wafanyabiashara, bali uwe rafiki na unaolinda thamani ya zao hili muhimu."

Mheshimiwa mgeni rasmi alisisitiza kuwa viongozi wa mikoa na halmashauri wanapaswa kuwa wabunifu katika kuanzisha vyanzo vya mapato ambavyo haviwadhuru wadau, bali vinaongeza tija, ufanisi na uendelevu wa sekta. Kwa ujumla hotuba ya mgeni rasmi ilisisitiza masuala makuu yafuatayo: zao la parachichi ni fursa kubwa kwa taifa, umuhimu wa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na wadau wa sekta binafsi ili kuendeleza na kulinda thamani ya parachichi na kwamba mfumo wa ukusanyaji wa mapato na ushuru lazima uendane na tija na usiwe kikwazo kwa wakulima au wasafirishaji/wanunuzi wa parachichi.



*"Zao la Parachichi ni Lulu ya Njombe," - Mhe. Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe na Mgeni Rasmi katika Mkutano wa Kitaifa wa Wadau wa zao la Parachichi. Mkutano huu ulifanyika katika hotel ya Agreement Njombe.*

# 3. Ujumbe wa Viongozi

**Salamu kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi.**

Kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Naibu Katibu Mkuu alisema kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wadau wa sekta ndogo ya parachichi ambao wamekuwa wakifanya jitihada katika kuendeleza zao hilo. Dkt Nindi alisisitiza kuwa jitihada hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kufanya zao la parachichi kuitwa "dhahabu ya kijani." Kadhalika, alibainisha kuwa Wizara ya Kilimo itaendelea kushirikiana na wadau hao katika kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazohusu tasnia hiyo.

Alibainisha kuwa wadau wa sekta binafsi wana nafasi muhimu katika kuishauri Serikali ili kuboresha mifumo ya uzalishaji na biashara, kwa lengo la kuhakikisha zao la parachichi linaendelea kuwanufaisha Watanzania na kuongeza mchango wake katika uchumi wa taifa. Aliendelea kusisitiza kuwa kama nchi bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kuhakikisha Tanzania inabaki kuwa mshindani mkuu kwenye masoko ya kimataifa ya parachichi, "hivyo kulifanya kombe libaki Tanzania na kuwanufaisha Watanzania kwa ujumla".

Dkt. Nindi pia alieleza juhudi za Serikali za kuanzisha COPRA, ikiwa ni hatua ya kutambua mchango wa mazao yasiyo na bodi. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza programu ya BBT katika kuimarisha huduma za ugani kwa zao la parachichi kwa lengo la kuchagiza huduma za ugani ili kuwafikia wakulima wengi. Dkt Nindi alimalizia kwa kusisitiza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, na kuhimiza kuendelea kufanya mambo nje ya utaratibu uliozoeleka, mtazamo ambao umekuwa msingi muhimu wa mafanikio ya tasnia ya parachichi nchini.




*Dkt. Stephe Nindi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo.*




**Salamu kutoka Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA**

Bi. Jacqueline Mkindi, Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA, kwa niaba ya Sekta Binafsi, alitoa shukrani kwa wadau wote wa umma na sekta binafsi kwa kushiriki mkutano huo muhimu wa kuweka vipaumbele, maono na ramani ya maendeleo ya tasnia kwa ujumla. Aidha, alieleza jinsi tasnia ya mazao ya bustani inavyoendelea kukua kwa kasi katika na hivyo kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuwa balozi mkubwa wa sekta hiyo.

Bi. Mkindi aliahidi kuwa TAHA itaendelea kushirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo pamoja na taasisi za COPRA, TPHPA, Halmashauri na wadau wote wa sekta binafsi. Alimalizia kwa kusisitiza kuwa matarajio ya sekta binafsi ni kuendeleza mashirikiano ya kimkakati na sekta ya umma ili kuhakikisha thamani ya parachichi la Tanzania inalindwa. Aidha, alitarajia kuwepo kwa umakini mkubwa katika kuanzisha na kutekeleza sera na mikakati mbalimbali itakayowezesha kukuza biashara badala ya kuzuia maendeleo ya sekta.

*Dkt. Jackline MKindi, Afisa Mtendaji Mkuu TAHA.*

# 4. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO WA KWANZA WA KITAIFA WA ZAO LA PARACHICHI APRILI, 2025

Wasilisho la utekelezaji kutoka COPRA.

Mkurugenzi Mkuu wa COPRA Bi. Irene M. Mlola alitoa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya mkutano ya mkutano wa kwanza wa wadau kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

| NA. | AZIMIO | UTEKELEZAJI | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Uratibu wa huduma za ugani (BBT Ugani). | COPRA inakamalisha taratibu za kuajiri vijana 50 kupitia mpango wa BBT-Ugani ambao kwa awamu ya kwanza watasambazwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe). | COPRA |
| 2 | Usimamizi wa ubora na usajili wa wadau wa mnyororo wa thamani, pamoja na uthibitishaji na elimu ya sheria ndogo. | COPRA imeandaa kanuni za usimamizi wa zao la parachichi chini ya Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 na zitaanza kutumika msimu mkubwa. Elimu itaanza kutolewa mwezi Novemba, 2025 kikanda (Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, na Magharibi). | COPRA |
| 3 | Kuratibu masoko na bei elekezi. | Urasimishaji wa uratibu wa masoko umekamilika ambao utaanza kutumika msimu huu. COPRA imeandaa wasilisho kuhusu bei anzia ambalo litawaslishwa katika mkutano huu. | COPRA |
| 4 | Usambazaji wa miche kwa mpango wa ruzuku. | COPRA itasambaza miche milioni moja kwa mpango wa ruzuku ambapo kwa awamu ya kwanza itasambazwa katika mikoa ya Nyanda za Juu kusini. COPRA ipo katika hatua za manunuzi (procument) za wazalishaji miche. Miche itaaanza kusambazwa mwishoni mwa mwezi Oktoba kwa wakulima watakaokuwa wamesajiliwa. | COPRA |

| NA. | AZIMIO | UTEKELEZAJI | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 5 | Usambazaji wa mbolea kwa mpango wa ruzuku | TFRA kwa kushirikia na TFC wameteua kampuni ya GUAVAY kusambaza tani 2,000 za mbolea aina ya HAKIKA NPK kwa Mpango wa Ruzuku kwa ajili ya zao la parachichi.<br>Aidha, utafiti wa mbolea maalum ya parachichi umekamilika kwa ushirikiano wa TARI, TFRA na kampuni ya ITRACOM na itaanza kusambazwa kwa Mpango wa Ruzuku kuanzia msimu huu wa kilimo kupitia TFC. | TFRA, TFC |
| 6 | NirC kuchimba visima vitakavyotumika kwenye umwagiliaji wa mashamba ya Parachichi. | Katika bajeti ya mwaka 20225/2026 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kuwezesha wakulima wa parachchichi kupata miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yao. | NirC |
| 7 | TPHPA kutoa viuatilifu vya zao la parachichi kwa mpango wa ruzuku | TPHPA imesambaza lita 8,800 za viuatilifu mbalimbali kwa wakulima kwenye maeneo ya uzalishaji kwa mpango wa ruzuku. | TPHPA |
| 8 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuanzisha Vyama vya Ushirikas vya zao la parachichi. | Uhamasishaji umefanyika ambapo jumla ya Vyama vya Ushirika sita (6) vimetanua wigo kwa kubadilisha masharti yao na kuongeza zao la parachichi hivyo kufanya vyama 37 vyenye jumla ya wanachama 4,048 kutoka 31 vilivyokuwepo awali katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa na Kagera. | TCDC |

# 4.1. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KUTOKA TFRA, TOSCI, NIRC & TCDC

Wawakilishi wa taasisi hizi walitoa taarifa za utekelezaji wa mkutano huo kama ifuatavyo:

2.2.1 TFRA

TFRA ilieleza kuwa, kwa kushirikiana na kiwanda cha Itracom Industries, mbolea maalum kwa zao la parachichi zimezalishwa kupitia kiwanda hicho ambazo ni Fomi Jr kwa miche midogo na Fomi Super kwa miti mikubwa na zitauzwa kwa bei ya ruzuku.

2.2.2 TOSCI

TOSCI ilieleza kuhusu utambuzi wa aina tano (5) za parachichi ambazo ni: Hass, Pinkerton, Fuerte, Ex - Kulu na Booth 7. Aidha, ilielezwa kuwa aina hizo zimeshasajiliwa. Vilevile, ilieleza kuwa jumla ya wazalishaji wa miche 625 wameshasajiliwa nchini.

2.2.3 NiRC

NiRC ilitoa taarifa kuhusu sababu za kuchelewa kwa huduma ya kuchimba visima katika mashamba ya parachichi ambayo ni changamoto ya upatikanaji vifaa. Ilielezwa kuwa Tume itachimba visima vya bure kwa vikundi vya wakulima wenye ekari 40 au zaidi na wakulima wadogo watachimbiwa kwa ruzuku ya asimilia 80 Aidha, ilielezwa kuwa, Tume hiyo itahakikisha mitambo inasambazwa kwenye mikoa husika kwa ajili ya uchimbaji wa visima kwa ajili ya wakulima wa parachichi.

2.2.4 TCDC

TCDC ilieleza kuwa itaendelea kuhamasisha wakulima kuanzisha vyama vya ushirika vya parachichi. Ilielezwa kuwa jumla ya vyama vya ushirika 37 vyenye jumla ya wanachama 4,048 vimeongeza wigo na kuongeza zao la parachichi katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa na Kagera.Kadhalika, Tume itashirikiana na Halmashauri katika maeneo ya uzalishaji wa zao la parachichi katika kutoa mafunzo ya uongezaji thamani wa parachichi.





Wadau mbalimbali wa zao la Parachichi wakifuatilia mawasilisho mbalimbali wakati wa kikao cha wadau wa zao hilo kilichofanyika Mkoa wa Njombe

# 5. Mawasilisho

## 3.1 Wasilisho kuhusu Urasimishaji wa Biashara ya Parachichi – COPRA

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Dkt. Yasinta Nzogela aliwasilisha mada kuhusu urasimishaji wa biashara ya parachichi. Dkt. Yasinta alieleza kuhusu COPRA kuanzisha kanuni ya usimamizi wa zao la Parachichi kama hatua muhimu ya urasimishaji wa shughuli katika mnyororo wa thamani wa parachichi, ikiwemo biashara ya parachichi
Dkt Yasinta alieleza lengo la urasimishaji ni kuimarisha usimamizi wa tasnia hiyo kwa manufaa ya wadau wote katika mnyororo wa thamani. Aidha, alieleza maeneo makuu ya utekelezaji wa Kanuni za Parachichi kama ifuatavyo;

### *Utekelezaji Kanuni za Parachichi*

- Ufunguzi wa msimu (msimu mdogo na msimu mkubwa),
- Matumizi ya kalenda ya msimu wa ununuzi,
- Usajili wa wadau (wanunuzi, wakala wa ununuzi),
- Utambuzi na usajili wa wavunaji,

### *Utekelezaji Kanuni za Parachichi*

- Utaratibu wa kupata vibali vya kuvuna na kusafirisha parachichi,
- Utambuzi na matumizi ya madaraja (Daraja la kwanza, Daraja la pili, Daraja la viwandani ( Kiambatisho Na.3),
- Kuanzishwa kwa vituo rasmi vya ununuzi wa parachichi, na
- Usimamizi wa bei ya parachichi.

Dr. Yasinta alimalizia kwa kusema kuwa, COPRA itatoa mafunzo kwa wadau wote ili utekelezejai wa kanuni hizo pamoja na masuala yaliyoainishwa.
Aidha, katika kuimarisha huduma za ugani, COPRA itaajiri maafisa ugani kupitia programu ya BBT–Ugani (Building a Better Tomorrow – Extension Services). Vijana hao ni wahitimu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na vyuo vingine vya kilimo watapatiwa mafunzo rejea na kusambazwa kwenye maeneo ya uzalishaji wa parachichi kwa lengo la kutoa huduma za ugani kwa wakulima na ili kuchochea ongezeko la tija na ubora kupitia usimamizi wa kanuni hizo.



## 3.2 Wasilisho kuhusu ‘Compliance’ ya Soko la Parachichi - TPHPA

Mwasilishaji alitoa taarifa kuhusu matakwa ya masoko ya kimataifa, akieleza kuwa kila soko lina vigezo vya ubora vinavyohitaji kufuatwa kabla ya usafirishaji. Alieleza kuwa hatua za pest analysis na traceability zimeanza kutekelezwa kupitia tafiti katika maeneo ya uzalishaji kama hatua mojawapo ya kukidhi matakwa ya masoko.

## 3.3. Wasilisho kuhusu Hali ya Masoko –TAHA

Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA alieleza kuwa, tasnia ya parachichi imeendelea kukua kwa kasi, ikichangia ongezeko la mapato ya wakulima na pato la taifa. Alisisitiza umuhimu wa elimu kwa wakulima kuhusu kuzingatia madaraja ya ubora na uthibiti (certification) ili kuongeza thamani ya mazao. Aidha, alieleza kuwa Tanzania imekuwa miongoni mwa wauzaji wakubwa wa parachichi barani Afrika, ikizishinda baadhi ya nchi kama Israel na Spain katika soko la Afrika Kusini, India na Ulaya. Alisema, usafirishaji wa parachichi nje ya nchi umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 101, kutoka tani 17,711 mwaka 2021/22 hadi tani 35,627 mwaka 2023/24. Hili ni ushahidi wa wazi kuwa tasnia hii ina nguvu kubwa. Ni muhimu kwa wadau wote kuchukua hatua madhubuti kuweka vipaumbele na dira ya pamoja ili kuongeza uzalishaji na ushindani wa parachichi ndani na nje ya nchi. Alimalizia kwa kusema, TAHA itaendelea kushirikiana na wadau kuendeleza na kulinda tasnia hii kupitia sera na mikakati inayoongoza sekta binafsi.

## 3.4. Wasilisho kuhusu Usimamizi wa Bei Anzia – COPRA

Bw. Kamwesige Mtembei, Mkurugenzi wa Idara ya Oparesheni na Udhibiti Ubora kutoka COPRA aliwaslisha kuhusu namna COPRA itakavyosimamia bei anzia sambamba urasimishaji wa usimamizi wa biashara ya parachichi nchini. Alieleza namna mjengeko wa bei anzia unavyoweza kupatikana hapa nchini kuwa ni gharama ya uzalishaji kutoka kwa mkulima, vituo vya kufangasha, tozo mbalimbali na gharama za usafirishaji.
Mkurugenzi Kamwesige alisema kuwa, katika hatua za suala zima la urasimishaji wa biashara ya parachichi hapa nchini, COPRA itakuwa inatoa bei anzia ya parachichi kila wiki katika msimu mkubwa kwa kufuata madaraja ya uzalishaji ambapo wasimamizi watakuwa ni Mikoa na Halmashauri katika maeneo ya uzalishaji. Utekezaji wake utahusisha kuundwa kwa kamati maalum ya upangaji bei anzia ambayo itakuwa inajadiliana kabla ya Kikao cha Wadau Mwanzoni mwa msimu.

Aliendelea kusema, COPRA inasisitiza kuwa kila mfanyabiashara wa zao la parachichi kununua kwa kufuata bei anzia itakayokuwa ikitolewa kila wiki kulingana na kanda/mikoa ya uzalishaji, aidha alimalizia kwa kueleza kuwa, mdau yeyote atakayekiuka au kuenenda biashara  kinyume na utaratibu, sheria itafuata mkondo wake.



# 6. MAJADILIANO

Katika mjadala wa pamoja, hoja na maoni mbalimbali ya kisera na kiutendaji yalitolewa na wadau. Miongoni wa maeneo yaliyojadiliwa ni:

## *Maeneo*

- Magonjwa ya parachichi,
- Mikopo kwa wakulima wa parachichi,
- Masuala ya uthibitishaji (certification),
- Changamoto ya umiliki wa ardhi kwa wakulima,
- Ujumuishaji wa masoko Market Integration, na Avocado Market Hub, na
- Makampuni ambayo hayazingatii masharti.

# 7. MAAZIMIO

Baada ya majadiliano mbalimbali katika mkutano huo, masuala kadhaa yaliazimiwa kama inavyoonekana katika bangokitita (Kiambatisho na 4).

# 8. HITIMISHO

Mkutano wa wadau wa zao la parachichi umeonesha dhamira ya pamoja ya Serikali na wadau wa sekta binafsi kuendeleza zao la parachichi kama eneo muhimu la kukuza uchumi wa kilimo nchini. Masuala yaliyojadiliwa yaliweka msisitizo katika kuongeza uzalishaji, kuimarisha ubora, kuboresha mifumo ya masoko na kuongeza ushindani katika soko la kimataifa.

Kauli ya Naibu Katibu Mkuu, Dkt Stephen Nindi, kuhusu kufanya “Biashara isiyo ya Mazoea” (Business Unusual)” imetoa mwongozo wa kimkakati kwa wadau wote kuongeza ubunifu, kuboresha utendaji na kuwekeza katika teknolojia na mifumo ya kisasa. Serikali imethibitisha kuendelea kuweka mazingira wezeshi kupitia kuweka ruzuku, sera rafiki na usimamizi wa viwango, ili sekta hii iendelee kukua kwa tija na kuwa chanzo kikuu cha mapato, ajira na fedha za kigeni.

# Washirika:

# Wadhamini:

**Mawasiliano:**

Mamlaka ya Udhibiti Nafaka na Mazao
Mchanganyiko
Jengo la Kahawa
Barabara ya Kahawa
S.L.P 2780
Dodoma, Tanzania
info@copra.go.tz
Piga bure: 0800117777

## Shirikisha, Boresha, Endeleza

# MAJADILIANO NA MAAZIMIO YALIYO AFIKIWA KATIKA KIKAO CHA WADAU WA ZAO LA PARACHICHI

**Septemba 25, 2025**

**Njombe**

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYO AFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ufunguzi rasmi wa msimu wa ununuzi wa parachichi. | COPRA kuendelea kuratibu ufunguzi wa misimu ya ununuzi wa parachichi. | Ufunguzi rasmi wa msimu mdogo wa ununuzi wa parachichi kwa mwaka 2025/2026 ulifunguliwa rasmi tarehe 25 Septemba, 2025.<br>Tanzania ina misimu miwili ya ununuzi wa parachichi. Msimu mdogo unaoanza Septemba hadi Novemba, na msimu mkubwa unaoanza Desemba hadi Juni. | COPRA kutangaza msimu mkubwa wa ununuzi mwezi DIsemba. | COPRA, Halmashauri, Wadau Wakulima |
| 2 | Urasimishaji wa tasnia ya zao la parachichi nchini. | COPRA kuanza kuweka mfumo rasmi wa usimamizi wa uzalishaji, usindikaji na biashara kupitia kanuni za Usimamizi wa Zao la Parachichi. Mfumo utahusisha usajili na utambuzi wa wadau na kutoa miongozo ya uzalishaji, ubora, usindikaji na biashara ya parachichi. | Kanuni za usimamizi wa zao la parachichi zimetambulishwa rasmi kwa wadau katika mkutano wa tarehe 25 Septemba, 2025. | Usajili wa wakulima, wakala wa ununuzi na wanunuzi wa parachichi kuanza rasmi Novemba, 2025.<br><br>Kuwatambua wavunaji/wachumaji wa parachichi ifikapo Desemba, 2025. | COPRA, Halmashauri TAHA, Wadau na Wakulima |
| 3 | Kuwa na kalenda ya kitaifa ya uvunaji. | Kalenda ya kitaifa ya uvunaji wa parachichi itasaidia kuepusha migongano ya soko. | Rasimu ya kalenda iliwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kuweka maoni na kuridhia. | Maboresho ya kalenda yanaendelea kwa kushirikiana na wadau, kazi hii itakamilika Desemba, 2025. | COPRA, Halmashauri TAHA, Wadau wengine na Wakulima |

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYOFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Kuanzishwa kwa Umoja wa Wasafirishaji wa parachichi (Exporters Association). | Wasafirishaji waliomba kusaidiwa kurasimisha umoja wao. | Lilipokelewa kwa ufuatiliaji. | Kutafuta taarifa kuhusu utaratibu wa urasmishaji. | COPRA<br>Wasafirishaji |
| 5 | Ufafanuzi wa madaraja ya parachichi. | Uelewa mdogo kuhusu utambuzi wa madaraja (Daraja la kwanza, Daraja la pili na Daraja la viwandani) kwa wadau katika tasnia. | Madaraja matatu ya parachichi kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Usimamizi wa Zao la Parachichi yaliwasilishwa katika kikao cha wadau cha tarehe 25 Septemba, 2025 kwa ajili ya uelewa. | Kutoa mafunzo ya kanuni za Usimamizi wa Zao la Parachichi kwa wadau – kanuni zitakapokamilika. | COPRA<br>Halmashauri<br>TAHA |
| 6 | Kuchelewa kwa shehena za parachichi katika bandari ya Dar es Saalam. | Shehena za parachichi kukaa muda mrefu katika bandari ya Dar es Salaam hivyo kuongeza gharama kwa wasafirishaji. | Limepokelewa kwa ufuatiliaji. | Hoja itawasilishwa TPA. | COPRA<br>TPA<br>Wadau |
| 7 | Usimamizi wa bei ya parachichi. | Wanunuzi wa parachichi wamekuwa wakipanga bei ya zao hilo kulingana na matakwa yao, jambo linalosababisha wakulima kushindwa kupata bei yenye uwiano na haki. | COPRA imetangaza kuundwa kwa kamati maalum itakayojumuisha wakulima, wanunuzi na Serikali kwa ajili ya kutangaza bei anzia pale itakapolazimu. Bei hiyo itahuishwa kila wiki kwa kuzingatia mwenendo wa soko la ndani na nje ya nchi. | Uundaji wa kamati maalum utakamilika ifikapo Desemba, 2025. | COPRA<br>Wizara ya Kilimo<br>Halmashauri<br>TAHA<br>Wadau<br>Wakulima |

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYO AFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Uwekezaji katika miundombinu ya usimamizi wa parachichi baada ya kuvuna. | Uhitaji wa maboresho ya vituo vya ukusanyaji na uhifadhi wa parachichi (collection centres) na maghala ya kufungashia parachichi (packhouses). | Katika mwaka 2025/2026 COPRA imetenga Shilingi bilioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa *collection center* 50 katika maeneo ya uzalishaji. | Maeneo nane (8) ya ujenzi wa vituo hivyo yametambuliwa katika Wilaya ya Rungwe, Utambuzi wa maeneo katika Mikoa na Wilaya nyingine utakamilika Desemba, 2025. | COPRA<br>Wizara ya Kilimo<br>Halmashauri |
| 9 | Hitaji la huduma za umwagiliaji katika mashamba ya parachichi. | Serikali kuharakisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya parachichi ili kuongeza tija na ubora wa zao hilo. | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itachimba visima vya maji bure kwa vikundi vya wakulima wenye ekari 40 au zaidi, na kwa Mpango wa Ruzuku ya asilimia 80 kwa wakulima wadogo.<br>Uchimbaji wa visima unatekelezwa kwa awamu ambapo tume imejipanga kuendelea kuyafikia maeneo mengine ya uzalishaji. | Ufuatiliaji utafanyika ili kupata mahitaji kutoka katika maeneo ya uzalishaji na kuyawasilisha NiRC. | COPRA<br>NirC<br>Wizara ya Kilimo<br>Halmashauri |
| 10 | Uhaba wa huduma za ugani katika maeneo ya uzalishaji. | Huduma za ugani zinahitajika kutolewa kwa wakulima kuanzia hatua ya kuandaa shamba hadi uvunaji ili kuhikisha uzalishaji unaofuata kanuni za kilimo bora (GAP). | COPRA itasambaza maafisa ugani 50 ambao ni wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na vyuo vingine vya kilimo kupitia programu ya BBT Ugani kuanzia Novemba 2025 ambapo kwa awamu ya kwanza mafisa ugani hao watasambazwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. | Vijana hao wamedahiliwa, wamepatiwa mafunzo na kusambazwa katika mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Ruvuma na Rukwa. | COPRA<br>Halmashauri<br>Wakulima |
| 11 | Ubovu wa barabara za mashambani na changamoto ya upatikanaji wa umeme vijijini. | Kuboresha barabara za mashambani na kuongeza upatikanaji wa huduma ya umeme vijijini kwa ajili ya shughuli za kilimo na uhifadhi wa mazao ili kuongeza uzalishaji na kulinda ubora wa | Kwa ufutatiliaji. | Ufuatiliaji unaendelea. | COPRA<br>TARURA<br>Halmashauri |

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYO AFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | Hitaji la upembuzi na utafiti wa masoko ya nje ( market intelligence). | Kupata taarifa sahihi za masoko (hususan ya nje) zitakazosaidia wadau kufanya maamuzi sahihi. | COPRA itaunda kamati maalum itakayoshirikisha wadau wote, lengo ni kufanya utafiti wa masoko ya parachihi katika soko la dunia. Taarifa za masoko na bei zitatolewa kila wiki. | Uundaaji wa kamati ya kufuatilia masoko na bei ya parachichi katika soko la nje utakamilika Desemba, 2024. | COPRA<br>Wizara ya Kilimo<br>TAHA<br>Wadau |
| 13 | Tozo na ushuru usio na uwiano na kutokuzingatiwa kwa leseni za daraja (class) la A, B na C katika baadhi ya maeneo. | Hitaji la kufanyika mapitio ya tozo na ushuru mbalimbali katika tasnia ya zao la parachichi ili kurahisisha biashara. Kuhakikisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni unazingatiwa ipasavyo; kutoa mafunzo kwa Halmashauri kuhusu aina za leseni na matumizi yake. | Kwa ufuatiliaji. | Ufuatiliaji utafanyika TAMISEMI kuhusu kutafuta suluhu ya jambo hilo kwa pamoja. | COPRA<br>Wizara ya Fedha<br>TAMISEMI |
| 14 | Kutokuwepo kwa ukaguzi wa mizani na upimaji sahihi sokoni. | Kuimarisha ukaguzi wa mizani na kutoa vyeti vya uthibitisho wa vipimo sahihi katika masoko. | Kwa ufuatiliaji. | Ufuatiliaji utafanyika Mamlaka ya Wakala wa Vipimo. | COPRA<br>WMA |
| 15 | Pembejeo za ruzuku | Wakulima waliomba Serikali kuendelea kutoa ruzuku za miche bora, viuatilifu na mbolea katika mikoa yote ya uzalishaji kutokana na bei kubwa ya pembejeo hizo. | Miche milioni 1 itaanza kuuzwa kwa Mpango wa Ruzuku Nyanda za Juu Kusini kwa awamu ya kwanza hadi kufikia miche milioni 2 katika maeneo yote ya uzalishaji. | Taratibu za ununuzi wa miche zinaendelea; COPRA itaendelea kufanya ufuatiliaji wa pembejeo za Mpango wa Ruzuku taasisi za TPHPA na TFRA. | COPRA<br>Wizara ya Kilimo<br>TPHPA<br>TFRA |

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYO AFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | Mikutano ya wadau ifanyike kwa mzugunguko. | Kuwa na mzugunguko wa mahali pa kufanyia mkutano ya wadau ili kuwafikia wadau wote katika maeneo ya uzalishaji. | Mikutano itakuwa inafanyika katika kwa mzunguko katika mikoa ya uzalishaji. | COPRA itatekeleza kwa kushirikiana na wadau. | COPRA<br>Halmashauri<br>Wadau<br>TAHA |
| 17 | Takwimu za maendeleo ya tasnia ya parachichi. | Kuanzisha mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa takwimu za uzalishaji, biashara na masoko ya parachichi katika ngazi ya taifa na mkoa. | COPRA inaenedelea kuandaa mfumo utakaowezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za zao la parachichi kwa kushirikiana na wadau na taasisi zingine. | Ujenzi wa mfumo unaendelea. | COPRA<br>Halmashauri<br>TAHA |
| 18 | Uuzaji holela wa parachichi mipakani. | Kudhibiti uuzaji usio rasmi kwa kuweka vituo maalum vya mauzo mipakani na kuimarisha ufuatiliaji wa vibali vya mauzo nje. | COPRA itajenga masoko ya mauzo ya mazao ya kilimo likiwemo zao la parachichi kwenye mipaka ya Kanda ya Ziwa katika awamu ya kwanza. | Taratibu za awali kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. | COPRA<br>Wizara ya Kilimo<br>Halmashauri |
| 19 | Akaunti za kigeni kwa Kampuni za usafirishaji. | Kuweka utaratibu wa makampuni yote ya mauzo ya nje kuwa na akaunti za kigeni ndani ya nchi ili kuongeza mapato ya taifa. | COPRA imeaandaa Kanuni za Usimamizi wa zao la parachichi zinazotoa mwongozo kuhusu hitaji la kampuni za kigeni ndani ya nchi. | Usimamizi wa utekelezaji utafanyika kwa kufuata mwongozo wa Kanuni za Usimamizi wa zao la Parachichi zitakapokamilika. | COPRA<br>Wadau |

# MASUALA YALIYOJADILIWA, MAAMUZI YALIYO AFIKIWA NA HATUA ZIFUATAZO

| Na. | SUALA | MAELEZO | UTEKELEZAJI | HATUA IFUATAYO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 20 | Vibali vya haraka vya Usafirishaji kwa Wauzaji Waliothibitishwa | Wauzaji wenye cheti cha Global GAP wanapaswa kupewa vibali vya usafirishaji kupitia mtandao wa kidigiti kwa kila shehena (consigniment), badala ya kuomba kwa kontena nyingi kwa wakati mmoja kwa kuwa inasababisha ucheleweshaji. | Maoni yamepokelewa | COPRA inaendelea kuboresha mfumo na tararatibu za utoaji wa vibali ili kuharakisha huduma. | COPRA<br>Wadau |
| 21 | Kuchapisha data za usafirishaji/mauzo ya parachichi kila wiki. | COPRA ianze kuchapisha takwimu za usafirishaji wa parachichi kila wiki kwenye tovuti yake ili kuvutia wawekezaji na wanunuzi wa kimataifa wanaohitaji takwimu za usafirishaji kwa wakati halisi (real time data). | Maoni yamepokelewa. COPRA inajukumu la kukusanya taarifa, hii itasaidia uwazi na kuboresha taarifa kwa wadau. | Uboreshaji wa mifumo ya kuapata taarifa sahihi na kwa wakati unaendelea. | COPRA<br>TAHA<br>Wadau |

MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO

Shirikisha, Boresha, Endeleza

COPRA

CEREALS AND OTHER PRODUCE REGULATORY AUTHORITY